JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA MAJI NA UMWAGILIAJI

MAJI VIJIJINI

MWONGOZO WA KUTATHMINI KAZI YA UFANISI WA JUMUIYA ZA WATUMIAJI MAJI.

MACHI, 2017

Yaliyomo

1.0 UTANGULIZI.

Ushirikishwaji wa Wananchi katika kusimamia na kuendeleza Miradi ni muhimu sana. Usimamizi huo hufanywa na jumuiya zilichosajiliwa Kisheria chini ya Sheria namba 12 ya Mwaka 2009. Jumuiya hii inawakilisha Wananchi. Ili kuwa na ufanisi jumuiya hii ni muhimu kufanyiwa ufuatiliaji na tathmini ili kuhakikisha taratibu na kanuni za uendeshaji zinafuatwa.

Dhumuni kubwa la ufuatiliaji na tahmini ya utendaji kazi wa jumuiya hizi ni kuhamasisha na kuimarisha uendeshaji wa miradi ili kuifanya iwe endelevu na yenye manufaa na tija kwa wananchi. Ufanisi wa jumuiya ya watumiaji maji inatofautiana kutokana na vigezo mbali mbali vinavyopelekea mgawanyo wa jumuiya za watumiaji maji katika makundi ili kuhakikisha tathimini ya utendaji kazi inafanywa kwenye jumuiya zenye sifa zinazoendana.

1.1 Dhana ya Mgawanyo wa jumuiya za Watumia Maji;

Mgawanyo Jumuiya za watumia maji ni mchakato wa kutenga Jumuiya za Watumia Maji katika madaraja tofauti tofauti, kwa ajili ya kurahisisha tathmini ya kiwango cha ubora wa utendaji kazi.

1.2 Vigezo vya Mgawanyo

Katika Mwongozo huu mgawanyo wa Jumuiya za Watumiaji Maji utatumia kigezo cha Teknolojia ya uzalishaji na usambazaji wa huduma ya maji. Kwa kigezo hiki kutakuwa na makundi mawili ya Jumuiya za Watumiaji Waji kwa minajiri ya tathmini.

Kundi la Na. 1 Ni miradi ya msukumo

Kundi la Na. 2 Ni miradi ya mtiririko

1.3 Mgawanyo

Kuna jumuiya ya watumiaji maji ambayo zina miradi mbalimbali, na tofauti tofauti katika asili, kwa mfano zipo Jumuiya za watumia maji zenye miradi yenye mfumo wa kusukuma, Jumuiya nyingine zina mchanganyiko wa miradi yenye mfumo wa kusukuma na kutiririka, pia kuna Jumuiya zenye miradi ya kutirirka tu.

Kundi Na. 1 ni miradi ya msukumo.

 -Jumuiya zenye miradi ya mfumo wa msukumo kutoka chanzo ambayo inajumuisha miradi inayotumia Mafuta, Nguvu ya jua, Umeme wa *Grid* kuu. Nishati ya upepo na pampu ya mkono. n.k

Kundi Na. 2 ni miradi ya mtiririko.

 -Jumuiya zenye mfumo wa mtiririko kutoka kwenye chanzo.

Zingatia; Jumuiya zenye miradi inayotumia mifumo yote miwili (Msukumo na mtiririko) mgawanyo wake utazingatia ni mfumo upi unaohudumia watu wengi zaidi

2.0 TATHIMINI YA UTENDAJI KAZI

Baada ya kupata madaraja mbalimbali yenye angalau sifa zinazofanana, zoezi zima la tathimini litakuwa jepesi kwani ni vizuri kupima uwezo wa Jumuiya vyenye tabia zinazowiana.

Sasa basi tathimini hii ya Jumuiya za watumia maji itafanywa kwa kuzingatia vigezo mbalimbali ambavyo kwa pamoja vinalenga suala zima la uendelevu wa miradi ikiwa ndio dhumuni kuu la zoezi hili.

2.1 Tathmini ya Jumuiya zenye Miradi ya Mtiriko.

Jedwali Na.01

Kigezo kikuu *(Main criteria)*	Vigezo vidogo *(Sub criteria)*	*(Set target)*	Uzito wa kigezo (%)	Uthibitisho wa taarifa (*Means of verification*)
Uongozi (Governance) 20%	**1. Muundo wa utawala** *(Organisation structure)*	Muundo wa utawala umezingatiwa = 1 Muundo wa utawala haujazingatiwa = 0	1%	
	2. Usajili	Jumuiya za watumiaji maji zenye namba ya usajili = 2, zilizokwishaanza mchakato wa usajili lakini bado hakijakamilisha = 1, Ambacho bado hakijaanza= 0	2%	
	3. Sifa za viongozi kielimu	Viongozi wote wana sifa za kielimu zilizoelezwa = 2, Angalau nusu ya idadi ya Viongozi wana sifa za Kielimu zilizoelezwa = 1, Viongozi wenye sifa ni chini ya nusu ya idadi ya viongozi = 0	2%	
	4. Kufanya mikutano mara kwa mara.	Kama Idadi ya mikutano iliyofanyika kwa mwaka ni 10-12 = 4, 7-9 = 3, 4-6 = 2, 1-3 = 1, 0 = 0.	4%	
	5. Uwepo wa ofisi	Ofisi inayomilikiwa na Jumuiya = 2, Ofisi kupanga/ kupewa ofisi =1, Hakuna kabisa ofisi = 0	2%	
	6. Usawa wa kijinsia miongoni mwa viongozi	Uwiano wa Ke/Me miongoni mwa viongozi ni nusu kwa nusu = 2, Kuna jinsia zote miongoni mwa viongozi lakini si kwa uwiano wa nusu kwa nusu =1, Kuna jinsia moja tu miongoni mwa viongozi = 0	2%	
	7. mahusiano ya Jumuiya cha watumiaji maji katika ngazi zote yaani Wananchi,	Jumuiya za Watumiaji Maji zinatoa taarifa katika ngazi zote = 3, Kinatoa katika ngazi mbili tu = 2,		

	Serikali ya Kijiji na CWST/Halmashauri	Kinatoa katika ngazi moja tu = 1, Hakitoi kabisa = 0.	3%	
	8. Uwezo kutatua migogoro	Migogoro yote iliyotokea imetatuliwa = 2, Angalau nusu ya idadi ya migogoro iliyotokea imetatuliwa = 1, Zaidi ya nusu ya idadi ya migogoro iliyotokea haijatatuliwa = 0	2%	
	9. Ukaguzi wa hesabu wa Jumuiya cha watumiaji maji	Uwepo wa taarifa ya ukaguzi wa hesabu za Jumuiya za watumiaji maji iliyofanyika mara 2 kwa mwaka = 2, Mara 1 kwa mwaka = 1, Haujafanyika kabisa = 0.	2%	

Ufundi (Technical) – 20%	**1.Uwiano wa Kiasi cha maji kinachozalishwa na kinachowafikia watumiaji (Asilimia ya upotevu wa maji- non revenue water)**	Ikiwa upotevu wa maji ni 0-20% = 2 21%-50% = 1 Zaidi ya 50% = 0.	2%	
	2. Uwepo wa mafundi	Uwepo wa idadi ya mafundi ambayo ni toshelevu kwa ajili ya matengenezo.= 2 Uwepo wa mafundi ambao hawatoshi = 1 Kutokuwepo kwa mafundi kabisa = 0	2%	
	3. Idadi ya DP's zinazofanya kazi	Kama angalau 81% ya jumla ya DPs zilizopo zinafanya kazi = 5, Kati ya 61%-80% ya jumla ya DPs zilizopo zinafanya kazi =4 Kati ya 41%-60% ya jumla ya DPs zilizopo zinafanya kazi =3, Kati ya 21%-40% ya jumla ya DPs zilizopo zinafanya kazi =2 Kati ya 11% -20% ya jumla ya DPs zilizopo zinafanya kazi =1 Chini ya 10% ya DPs zote zilizopo zinafanya kazi. = 0	5%	
	4. Maji yaliyopimwa (metered DP)	Kama angalau 81% ya jumla ya DPs zilizopo zimefungwa mita = 2, Kati ya 41%-80% ya jumla ya DPs zilizopo zimefungwa mita = 1,	2%	

		Chini ya 41% ya jumla ya DPs zilizopo zimefungwa mita = 0		
	5. Urahisi wa upatikanaji Vipuri (*spare parts)* kwa ajili ya matengenezo	Uwepo wa stoo na vipuri muhimu toshelezi = 5,\ Uwepo wa stoo na vipuri muhimu vichache = 4, Uwepo wa stoo lakini hamna vipuri kabisa = 3, Jumuiya za watumiaji maji kisicho na stoo wala vipuri lakini vinapatikana maeneo jirani. (*within LGA*) = 2 Jumuiya za watumiaji maji zisizo na stoo wala vipuri lakini vinapatikana maeneo ya mbali (*Outside LGA)* = 1, Jumuiya za watumiaji maji zisizo na stoo wala vipuri na havipatikani kabisa (havipo ndani ya mkoa) = 0	5%	
	6.Utunzaji wa kumbukumbu za matengenezo	Jumuiya za watumiaji maji zenye kumbukumbu za matengenezo (*Maintenance schedules*) zinazozingatiwa = 2, Jumuiya za watumiaji maji zenye kumbukumbu za matengenezo (*Maintenance schedules*) lakini hazizingatiwi = 1, Jumuiya za watumiaji maji zisizo na kumbukumbu za matengenezo (*Maintenance schedules* = 0,	2%	
	7. Ubora wa maji	Jumuiya za watumiaji maji zinazoweka maji dawa kila siku na kupima ubora wa maji angalau mara 2 kwa mwaka = 2, Jumuiya za watumiaji maji zisizoweka maji lakini kinapima ubora wa maji angalau mara 2 kwa mwaka = 1, Jumuiya za watumiaji maji zisizoweka maji dawa wala kupima ubora wa maji = 0,	2%	

Fedha (Financial mgt) 25%	**1. Kiwango cha bei ya maji (Tarrif)**	Bei ya maji katika DPs inakidhi asilimia gani ya gharama za matengenezo: 81% -100% = 4 , 61% -80% = 3 , 41% -60% = 2 , 21% -40% = 1 , Chini ya 20% = 0 ,	4%	
	2. Kiwango cha ukusanyaji wa fedha	Kiwango halisi cha makusanyo kulinganisha na mauzo (collection efficiency): 81% -100% = 5 , 61% -80% = 4 , 41% -60% = 3 , 21% -40% = 2 , Chini ya 20% = 1 ,	5%	
	3. Matumizi sahihi ya fedha zilizokusanywa	Matokeo ya ukaguzi wa hesabu za Jumuiya za watumiaj maji iliyofanyika Taarifa zote 2 zinaonyesha Matumizi yalizingatia mwongozo wa fedha wa Jumuiya = 8-10, Taarifa 1 inaonyesha Matumizi yalizingatia mwongozo wa fedha wa Jumuiya = 6-7, Taarifa zote 2 zinaonyesha Matumizi hayakuzingatia mwongozo wa fedha wa Jumuiya = 4-5, Hakuna taarifa ya ukaguzi = 0-3	10%	
	4. Akaunti ya benki.	Akaunti ya benki iliyo hai na inatumika kulingana na mwongozo (mfano fedha za makusanyo zinapelekwa kila wiki/mwezi) = 3, Akaunti ya benki iliyo hai lakini haitumiki	3%	

		kulingana na mwongozo (mfano fedha za makusanyo haziwasilishwi kama ilivyopangwa) = 2, Akaunti ya benki ipo lakini fedha hazipelekwi kabisa = 1, Hakuna akaunti ya Benki = 0,		
	5. Utunzaji wa kumbukumbu za fedha	Jumuiya za watumiaji maji zenye vitabu vyenye kumbukumbu za fedha vinavyotumika = 2- 3, vitabu vya kumbukumbu za fedha vipo lakini havitumiki =1, vitabu vya kumbukumbu za fedha vipo lakini havitumiki =0,	3%	
Utendaji (Operations) 25%	**1. Uhusiano kati ya Taaluma ya mtumishi na nafasi aliyopo**	Jumuiya za watumiaji maji zitapewa alama kutokana na uwiano watumishi wenye taaluma sahihi dhidi ya jumla ya watumishi: 81% -100% = 5 , 61% -80% = 4 , 41% -60% = 3 , 21% -40% = 2 , Chini ya 20% = 1 ,	5%	
	2. Kuweza kutoa taarifa za mwezi kwa usahihi na kwa wakati	Jumuiya za watumiaji maji zitajipatia alama kutokana na utoaji wa taarifa zinazohitajika wa wakati (taarifa 12 kwa mwaka) Taarifa 9-10 = 6, Taarifa 7-8 = 5, Taarifa 5-6 = 4, Taarifa 3-4 = 3, Taarifa 2 = 2, Taarifa 1 =1, Taarifa 0= 0,	6%	
	3. Uwezo wa kuongeza DP's kuwa zaidi ya zilizopo kwa wanufaikaji	Idadi ya DPs zilizoongezeka ni asilimia ngapi ya zilizopo. Zaidi ya 20% = 6 11% -20% = 4,	6%	

		1%-10% = 2 0% = 0.		
	4. Kiwango cha watumiaji wanaonufaika kulingana na usanifu	uwiano wa wanufaikaji dhidi ya jumla ya wakazi katika eneo husika. 81% -100% = 5 , 61% -80% = 4 , 41% -60% = 3 , 21% -40% = 2 , Chini ya 20% = 1 ,	5%	
	5. Utunzaji wa kumbukumbu za uendeshaji wa mradi	Uwepo wa vitabu vya kumbukumbu za uendeshaji wa mradi kumbukumbu zote zinazotakiwa zipo na zinatunzwa vizuri = 3 kumbukumbu zilizopo ni chache na zinatunzwa vizuri = 2 kumbukumbu zilizopo ni chache na hazitunzwi vizuri = 1. kumbukumbu zote hazipo = 0.	3%	
Utunzaji na Uboreshaji/usafi wa Mazingira-10%	**1. Utunzaji wa mazingira**	Uwepo wa mikakati ya kutunza mazingira katika zanzo na vituo za maji. Mikakati ipo na imeshatekelezwa = 4, Mikakati ipo na inaendelea kutekelezwa = 3 Mikakati ipo na haijaanza kutekelezwa = 2 Mikakati bado inaaandaliwa = 1 Mikakati haipo = 0	4%	
	2. Utunzaji wa miundombinu ya mradi	Jumuiya za watumiaji maji zinazotunza miundo mbinu ya mradi (chanzo,Dps,Tank) Utunzaji unafanyika vizuri = 3, Utunzaji unafanyika lakini hauridhishi = 2, Utunzaji umepangwa lakin utekelezaji bado = 1 Hakuna mipango ya utunzaji = 0.	3%	

	3. Uendelezaji wa huduma ya maji	Jumuiya za watumiaji maji zilizo na mipango kutoa huduma endelevu ya maji (uboreshaji) Uendelezaji unafanyika vizuri = 3, Uendelezaji unafanyika lakini hauridhishi = 2, Uendelezaji umepangwa lakin utekelezaji bado = 1 Hakuna mipango ya Uendelezaji = 0	3%	

2.2 Tathmini ya Jumuiya Zenye Miradi ya Msukumo.

Jedwali Na.02

Kigezo kikuu *(Main criteria)*	Vigezo vidogo *(Sub criteria)*	*(Set target)*	Uzito wa kigezo (%)	Uthibitisho wa tarifa (*Means of verification)*
Uongozi (Governance) 20%	**1. Muundo wa utawala** *(Organisation structure)*	Muundo wa utawala umezingatiwa = 1 Muundo wa utawala haujazingatiwa = 0	1%	
	2. Usajili	Jumuiya za watumiaji maji zenye namba ya usajili = 2, zilizokwishaanza mchakato wa usajili lakini bado hakijakamilisha = 1, Ambacho bado hakijaanza= 0	2%	
	3. Sifa za viongozi kielimu	Viongozi wote wana sifa za kielimu zilizoelezwa = 2, Angalau nusu ya idadi ya Viongozi wana sifa za Kielimu	2%	

	zilizoelezwa = 1, Viongozi wenye sifa ni chini ya nusu ya idadi ya viongozi = 0		
4. Kufanya mikutano mara kwa mara.	Kama Idadi ya mikutano iliyofanyika kwa mwaka ni 10-12 = 4, 7-9 = 3, 4-6 = 2, 1-3 = 1, 0 = 0.	4%	Wananchi kushiriki kizuri katika kutoa maamuzi
5. Uwepo wa ofisi	Ofisi inayomilikiwa na Jumuiya = 2, Ofisi kupanga/ kupewa ofisi =1, Hakuna kabisa ofisi = 0	2%	
6. Usawa wa kijinsia miongoni mwa viongozi	Uwiano wa Ke/Me miongoni mwa viongozi ni nusu kwa nusu = 2, Kuna jinsia zote miongoni mwa viongozi laki si kwa uwiano wa nusu kwa nusu =1, Kuna jinsia moja tu miongoni mwa viongozi = 0	2%	
7. Mahusiano ya Jumuiya cha watumiaji Maji katika ngazi zote yaani Wananchi, Serikali ya Kijiji na CWST/Halmashauri	Jumuiya za watumiaji maji zinatoa taarifa katika ngazi zote = 3, Kinatoa katika ngazi mbili tu = 2, Kinatoa katika ngazi moja tu = 1, Hakitoi kabisa = 0.	3%	
8. Uwezo kutatua migogoro	Migogoro yote iliyotokea imetatuliwa = 2, Angalau nusu ya idadi ya migogoro iliyotokea imetatuliwa = 1, Zaidi ya nusu ya idadi ya migogoro iliyotokea haijatatuliwa = 0	2%	
9. Ukaguzi wa hesabu wa Jumuiya cha watumiaji maji	Uwepo wa taarifa ya ukaguzi wa hesabu za Jumuiya za watumiaji maji iliyofanyika mara 2 kwa mwaka = 2, Mara 1 kwa mwaka = 1, Haujafanyika kabisa = 0.	2%	

Ufundi (Technical) – 30%	**1.Uwiano wa Kiasi cha maji kinachozalishwa na kinachowafikia watumiaji (Asilimia ya upotevu wa maji- non revenue water)**	Ikiwa upotevu wa maji ni 0-20% = 3 21%-35% = 2 36%-50% = 1 Zaidi ya 50% = 0.	3 %	
	2. Uwepo wa mafundi	Uwepo wa idadi ya mafundi ambayo ni toshelevu kwa ajili ya matengenezo.= 5-8 Uwepo wa mafundi ambao hawatoshi = 1-4 Kutokuwepo kwa mafundi kabisa = 0	8 %	
	3. Idadi ya DP's zinazofanya kazi	Kama angalau 91% ya jumla ya DPs zilizopo zinafanya kazi = 6, Kati ya 81%-90% ya jumla ya DPs zilizopo zinafanya kazi =5 Kati ya 61%-80% ya jumla ya DPs zilizopo zinafanya kazi =4 Kati ya 41%-60% ya jumla ya DPs zilizopo zinafanya kazi =3, Kati ya 21%-40% ya jumla ya DPs zilizopo zinafanya kazi =2 Kati ya 11% -20% ya jumla ya DPs zilizopo zinafanya kazi =1 Chini ya 10% ya DPs zote zilizopo zinafanya kazi. = 0	6 %	
	4. Maji yaliyopimwa (metered DP)	Kama angalau 81% ya jumla ya DPs zilizopo zimefungwa mita = 3, Kati ya 41%-80% ya jumla ya DPs zilizopo zimefungwa mita = 2, Kati ya 21%-40% ya jumla ya DPs zilizopo zimefungwa mita = 1, Chini ya 21% ya jumla ya DPs zilizopo zimefungwa mita = 0	3 %	
	5. Urahisi wa upatikanaji Vipuri (*spare parts)* kwa ajili ya matengenezo	Uwepo wa stoo na vipuri muhimu toshelezi = 5-6, Uwepo wa stoo na vipuri muhimu vichache = 4, Uwepo wa stoo lakini hamna vipuri kabisa = 3,	6 %	

		Jumuiya za watumiaji maji zisizo na stoo wala vipuri lakini vipuri vinapatikana maeneo jirani. (*within LGA*) = 2 Jumuiya za watumiaji maji zisizo na stoo wala vipuri lakini vinapatikana maeneo ya mbali (*Outside LGA)* = 1, Jumuiya za watumiaji maji zisizo na stoo wala vipuri na havipatikani kabisa (havipo ndani ya mkoa) = 0		
	6.Utunzaji wa kumbukumbu za matengenezo	Jumuiya za watumiaji maji zenye kumbukumbu za matengenezo (*Maintenance schedules*) zinazozingatiwa = 2, Jumuiya za watumiaji maji zenye kumbukumbu za matengenezo (*Maintenance schedules*) lakini hazizingatiwi = 1, Jumuiya za watumiaji maji zisizo na kumbukumbu za matengenezo (*Maintenance schedules* = 0,	2 %	
	7. Ubora wa maji	Jumuiya za watumiaji maji zinazoweka maji dawa kila siku na kupima ubora wa maji angalau mara 2 kwa mwaka = 2, Jumuiya za watumiaji maji zisizoweka maji lakini kinapima ubora wa maji angalau mara 2 kwa mwaka = 1, Jumuiya za watumiaji maji zisizoweka maji dawa wala kupima ubora wa maji = 0,	2 %	
Fedha (Financial mgt) 25%	**1. Kiwango cha bei ya maji (Tarrif)**	Bei ya maji katika DPs inakidhi asilimia gani ya gharama za matengenezo: 81% -100% = 4 , 61% -80% = 3 , 41% -60% = 2 , 21% -40% = 1 , Chini ya 20% = 0 ,	4 %	

	2. Kiwango cha ukusanyaji wa fedha	Kiwango halisi cha makusanyo kulinganisha na mauzo (collection efficiency): 81% -100% = 5 , 61% -80% = 4 , 41% -60% = 3 , 21% -40% = 2 , Chini ya 20% = 1 ,	5 %	
	3. Matumizi sahihi ya fedha zilizokusanywa	Matokeo ya ukaguzi wa hesabu za Jumuiya za watumiaj maji iliyofanyika Taarifa zote 2 zinaonyesha Matumizi yalizingatia mwongozo wa fedha wa Jumuiya = 8-10, Taarifa 1 inaonyesha Matumizi yalizingatia mwongozo wa fedha wa Jumuiya = 6-7, Taarifa zote 2 zinaonyesha Matumizi hayakuzingatia mwongozo wa fedha wa Jumuiya = 4-5, Hakuna taarifa ya ukaguzi = 0-3	10 %	
	4. Akaunti ya benki.	Akaunti ya benki iliyo hai na inatumika kulingana na mwongozo (mfano fedha za makusanyo zinapelekwa kila wiki/mwezi) = 3, Akaunti ya benki iliyo hai lakini haitumiki kulingana na mwongozo (mfano fedha za makusanyo haziwasilishwi kama ilivyopangwa) = 2, Akaunti ya benki ipo lakini fedha hazipelekwi kabisa = 1, Hakuna akaunti ya Benki = 0,	3 %	
	5. Utunzaji wa kumbukumbu za fedha	Jumuiya za watumiaji maji zenye vitabu vyenye kumbukumbu za fedha vinavyotumika = 2- 3,		

		vitabu vya kumbukumbu za fedha vipo lakini havitumiki =1, vitabu vya kumbukumbu za fedha vipo lakini havitumiki =0,	3%	
Utendaji (Operations) 20%	**1. Uhusiano kati ya Taaluma ya mtumishi na nafasi aliyopo**	Jumuiya za watumiaji maji zitapewa alama kutokana na uwiano watumishi wenye taaluma sahihi dhidi ya jumla ya watumishi: 61% -100% = 3, 41% -60% = 2, 21% -40% = 1, Chini ya 20% = 0,	3%	
	2. Kuweza kutoa taarifa za mwezi kwa usahihi na kwa wakati.	Jumuiya za watumiaji maji zitajipatia alama kutokana na utoaji wa taarifa zinazohitajika wa wakati (taarifa 12 kwa mwaka) Taarifa 9-10 = 5, Taarifa 7-8 = 4, Taarifa 5-6 = 3, Taarifa 3-4 = 2, Taarifa 1-2 = 1, Taarifa 0= 0,	5%	
	3. Uwezo wa kuongeza DP's kuwa zaidi ya zilizopo kwa wanufaikaji	Idadi ya DPs zilizoongezeka ni asilimia ngapi ya zilizopo. Zaidi ya 20% = 5 11% -20% = 4, 1%-10% = 2 0% = 0.	5%	
	4. Kiwango cha watumiaji wanaonufaika kulingana na usanifu	uwiano wa wanufaikaji dhidi ya jumla ya wakazi katika eneo husika. 81% -100% = 4, 61% -80% = 3, 41% -60% = 2, 21% -40% = 1, Chini ya 20% = 0,	4%	

	5. Utunzaji wa kumbukumbu za uendeshaji wa mradi	Uwepo wa vitabu vya kumbukumbu za uendeshaji wa mradi kumbukumbu zote zinazotakiwa zipo na zinatunzwa vizuri = 3 kumbukumbu zilizopo ni chache na zinatunzwa vizuri = 2 kumbukumbu zilizopo ni chache na hazitunzwi vizuri = 1. kumbukumbu zote hazipo = 0.	3%	
Utunzaji na Uboreshaji/usafi Mazingira-5%	**1. Utunzaji wa mazingira karibu na vyanzo**	Uwepo wa mikakati ya kutunza mazingira katika vyanzo na vituo vya maji. Mikakati ipo na imeshatekelezwa = 2, Mikakati ipo na haijaanza kutekelezwa = 1 Mikakati bado inaaandaliwa/haipo = 0	2%	Kutofanyika kwa shughuli za kibinadamu karibu na maeneo ya vyanzo
	2. Utunzaji wa miundombinu ya mradi	Jumuiya za watumiaji maji zinazotunza miundo mbinu ya mradi (chanzo,Dps,Tank) Utunzaji unafanyika vizuri = 2, Utunzaji unafanyika lakini hauridhishi = 1, Utunzaji umepangwa lakin utekelezaji bado / hakuna mipango ya utunzaji = 0	2%	
	3. Uendelezaji wa huduma ya maji	Jumuiya za watumiaji maji zilizo na mipango kutoa huduma endelevu ya maji (uboreshaji) Mipango ya uendelezaji inafanyika vizuri = 1, Uendelezaji umepangwa lakin utekelezaji	1%	

		bado hakuna mipango ya Uendelezaji = 0		

Angalizo:

Ufundi kwenye tathmini ya miradi ya msukumo umepewa uzito zaidi (30%) kuliko kwenye miradi ya mtiririko (20%) kwa sababu vigezo vinavyotumika kutathmini ufundi kwenye miradi ya msukumo kuna mfumo/mifumo ya mashine ambayo inahitaji uwepo wa idadi kubwa ya mafundi wenye ujuzi unaohitajika pamoja na usimamizi wa karibu ili kuwezesha matengenezo na marekebisho yanayotokea mara kwa mara.

Utendaji kwenye tathmini ya miradi ya msukumo umepewa uzito mdogo (20%) kuliko kwenye miradi ya mtiririko (25%) kwa sababu vigezo vinavyotumika kutathmini utendaji vinaweza kufikiwa kirahisi kwenye miradi ya msukumo (mfano ni rahisi kufikisha maji maeneo yote ya mradi wa msukumo)

Utunzaji na Uboreshaji wa vyanzo vya maji umepewa uzito mkubwa (10%) kwenye miradi ya mtiririko kuliko kwenye miradi ya msukumo (5%) kwa sababu vigezo vinavyotumika kutathmini vinafanyika kwa kiasi kikubwa kwenye miradi ya mtiririko kuliko miradi ya msukumo.

3.0 HITIMISHO

Wizara inapendekeza Tathmini ya Jumuiya za Watumiaji maji ifanyike mara moja kila mwaka wa fedha. Tathmini hiyo itafanywa na Wizara kwa kupitia taarifa COWSO zitakazowasilishwa na Wahandisi wa Sekretarieti za Mikoa. Hata hivyo Halmashauri wanashauriwa kufanya tathmini kila baada ya robo mwaka, ili kufahamu uhalisia wa ufanisi wa vyombo vyao.